

ASb  
approved



# Msichana Aliyenuka

Brigid Simiyu

Catherine Groenewald

Kiswahili





Bahati alikuwa msichana mrembo na nyanyake alimpenda sana.




Nyanyake alitumia muda mrefu kumshonea Bahati sketi ya kuvutia. Bahati alipenda sana kuivaa sketi ile.




Wasichana wengine kijijini walimwonea wivu Bahati kwa sababu ya sketi hiyo. Walipanga kuificha. Lakini, ilikuwa vigumu kuichukuwa sketi hiyo akiwa ameivaa.



Asubuhi moja wasichana hao walimwalika Bahati aende kuogelea nao katika mto uliokuwa karibu. Walizivua nguo zao na kuziacha ukingoni ili zisitote. Kisha wakajitosa majini na kurushiana maji kwa muda.



Baada ya muda, walitosheka kuogelea. Kiongozi wa wasichana wenye wivu, aliirusha sketi ya Bahati majini, karibu na sehemu iliyokuwa na nyoka mkubwa. Halafu wasichana hao wengine waliondoka na kumuacha Bahati akilia kando ya mto.



Mara yule nyoka mkubwa akamsikia akilia. Alijichomoza na kumwona Bahati mrembo. Nyoka huyo alimmeza Bahati pamoja na ile sketi.




Nyoka yule hakuipenda ladha ya sketi, akaitema. Kwa bahati, akamtema Bahati pia. Bahati alilala ukingoni mwa mto huku amejifunika kwa sketi yake. Alikuwa amepakwa tope la kunata kutoka tumboni mwa nyoka. Tope hilo lilinuka fee.





Baadaye, Bahati aliivaa sketi yake iliyonuka na kukimbilia nyumbani.

Alipofika nyumbani, aliimba: Mama, nifungulie mlango, miye nanuka; Mama, nifungulie mlango, miye nanuka; Miye nanuka fee. Mama alipousikia wimbo wa Bahati, alitoka nje na kumjibu: Nenda zako Bahati, unanuka; Nenda zako Bahati, unanuka; Bahati, unanuka fee.



Bahati alihuzunika sana. Akakimbilia kwa mjombake na shangaziye.

Walimsikia akiimba: Nifungulieni mlango, miye ninanuka;  
Nifungulieni mlango, miye ninanuka; Miye ninanuka fee.  
Shangazi na mjomba walitoka nje wakiimba: Nenda Bahati,  
unanuka, Nenda Bahati, unanuka, Nenda! Nenda! Unanuka  
fee.




Bahati alibaki na wazo moja tu, kukimbilia nyumbani kwa nyanyake. Lakini, moyo wake ulikuwa mzito. Alijua hakuna aliyemtaka msichana aliyenuka fee.



Bahati alikuwa amekosea. Nyanyake hakumfukuza. Nyanya alimwosha, akaiosha sketi yake, akahakikisha kila kitu kilinukia.



Kutoka wakati huo, Bahati aliishi na nyanyake. Siku moja mvulana tajiri sana alitaka kumwoa Bahati.



Wazazi wa Bahati walipofahamishwa kuhusu jambo hilo,  
walitaka arudi kuishi nao.





Bahati alikumbuka jinsi walivyomchukia aliponuka fee. Aliwaambia, "Sitawahi kurudi nyumbani kwenu tena. Lazima wazazi wwapende watoto wao hata wakinuka."



Badala yake Bahati alimwalika nyanyake aende akaishi naye  
nyumbani mwa mvulana tajiri.





Nyanyake alifurahi sana, na wakaishi maisha raha mstarehe.

You are free to download, copy, translate or adapt this story  
and use the illustrations as long as you attribute in the  
following way: Southern African Folktale Author - Southern

African Folktale

Translation - Brigid Simiyu

Illustration - Catherine Groenewald

Language - Kiswahili

Level - Longer paragraphs © African Storybook Initiative

2014

Creative Commons: Attribution 4.0

Source [www.africanstorybook.org](http://www.africanstorybook.org)



